**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**
**MTIHANI WA KUHITIMU KIDATO CHA NNE**

**015** **ELIMU YA DINI YA KIISLAMU**
(Kwa Watahiniwa Walioko na Wasiokuwa Shuleni)

**Muda : Saa 3:00** **Mwaka: 2022**

**Maelekezo**

1. Karatasi hii ina sehemu A, B na C zenye jumla ya maswali **kumi na tatu (13)**.
2. Jibu maswali **yote** katika sehemu A na B na maswali **matatu (3)** kutoka sehemu C.
3. Sehemu A ina alama **ishirini (20)**, sehemu B alama **thelathini na tano (35)** na sehemu C ina alama **arobaini na tano (45)**.
4. Simu za mkononi na vitu vyote visivyoruhusiwa **havitakiwi** katika chumba cha mtihani.
5. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

2 101015 100025



Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org
CamScanner

## SEHEMU A (Alama 20)

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

1. Katika kipengele (i) – (xv), chagua jibu sahihi kisha andika herufi yake katika kijitabu chako cha kujibia.

(i) Elimu yenye manufaa kwa mujibu wa Uislamu inakuwa na sifa gani?

A Inahusisha Dini na dunia.
B Inafundisha ya Dunia na Akhera.
C Inawezesha kufanya Ibada.
D Inasababisha kupata ajira.
E Inatoa ujuzi na maarifa.

(ii) Kundi lipi linaonesha vigawe sahihi vya Tawhiid?

A Uluhiyyah, Rububiyyah na Asmaaiyya.
B Swifatiyya, Uluhiyyah na Rubbuubiyyah.
C Uluhiyyah, Asmaai waswifat na Ibadah.
D Uluhiyyah, Rububiyyah na Asmaai waswifat.
E Rububiyyah, Asmaaiyya na Swifaatiyya.

(iii) Kwanini Wahyi ni njia muhimu kwa watu kumjua Mwenyezi-Mungu (S.W)?

A Ni njia pekee ya kumjua Mwenyezi-Mungu (S.W)
B Ni njia ambayo haiwezi kubadilishwa kimaana.
C Ni njia ya kwanza iliyopo moyoni mwa watu.
D Ni njia inayofafanua wazi itikadi sahihi kwa watu.
E Ni njia pekee iliyotumiwa na Mtume (S.A.W)

(iv) Kwanini sio sahihi kuitafsiri Dini kama "Njia ya mahusiano kati ya mwanadamu na Mungu"?

A Zipo njia nyingine za kuhusiana na Mungu tofauti na dini.
B Tafsiri hiyo imetolewa na jamii ya wasiokuwa Waislamu.
C Tafsiri hiyo inaonesha kuwa, dini ni hiyari kwa wanadamu.
D Mwanadamu anahusiana na Mungu kiroho na haitaji dini.
E Tafsiri hiyo inaonesha kuwa dini ni lazima kwa wanadamu.

(v) Ibada ya Zakat na Sadaka inazingatia mambo mengi katika utekelezaji wake **isipokuwa**

A Kutoa vilivyo halali.
B Kutoa mwezi wa Ramadhani.
C Kutoa vilivyo vizuri.
D Kutoa kati kwa kati.
E Kujiepusha na Ria.

(vi) Kwa namna gani Uislamu unamuwezesha muumini kuwa katika ibada wakati wote wa maisha?

A Umelazimisha kutekelezwa kwa nguzo tano za Dini.
B Dhana ya ibada inahusu kila jambo katika Uislamu.
C Katika Uislamu kuna nguzo za Imani.
D Uislamu umeondoa uhuru wa watu kupumzika.
E Kuna majengo ya ibada za Waislamu katika nchi zote.



Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

CamScanner

(vii) Anapaswa kufanya nini mtu anayemsalia maiti baada ya Imam kuleta Takbira ya tatu?

A Kumuombea maiti.
B Kusoma Surat Fat'ha.
C Kutia Nia.
D Kusoma Sala ya Mtume.
E Kutoa Salaam.

(viii) Ufafanuzi wa mafundisho ya Uislamu kwa mujibu wa mabadiliko ya mazingira na wakati ni matokeo ya kutekelezwa kwa msingi gani wa Sharia?

A Ijtihaad
B Qur'an
C Sunna
D Qur'an na Sunnah
E Sunna na Hadithi

(ix) Ni kwa muktadha gani dhana ya Hadithi inafafanuliwa kama jambo au kitu kipya, taarifa au hotuba?

A Katika mazingira ya kisheria
B Kihistoria
C Katika mazingira ya kilugha
D Kimatumizi
E Katika kuifafanua Sunna

(x) Mafundisho gani mahususi yanayopatikana katika Suratul – Ikhlas?

A Shetani ni adui mkubwa wa mwanadamu.
B Kuna shari katika giza la usiku linapoingia.
C Uislamu ni njia sahihi ya maisha.
D Kazi kubwa ya Shetani ni kutia wasiwasi moyoni.
E Allah (S.W) ndio jina la dhati la Mwenyezi Mungu.

(xi) Jambo gani linaonesha wajibu wa mwanadamu wa kutafuta Dini sahihi katika maisha yake?

A Kuwepo kwa Dini nyingi duniani.
B Hitajio la mwanadamu kiroho.
C Uwezo wa mwanadamu kuamua.
D Kuletwa kwa Mitume wa Mungu.
E Kuwepo kwa midahalo ya kidini.

(xii) Kwa mujibu wa Uislamu, maumbile yote yaliyomzunguka mwanadamu yamewekwa duniani kwa malengo gani makubwa?

A Kuipamba dunia na anga.
B Kuweka usawa wa kiekolojia.
C Kuonesha uwezo wa kiuumbaji.
D Kumtumikia mwanadamu kimahitaji.
E Kuwa alama kwa malaika na watu.

(xiii) Hoja gani inabainisha lengo kuu la kusoma historia kiutendaji?

A Kuona asili na hadhi yetu.
B Kujikumbusha yaliyopita.
C Kupata mafunzo na kujirekebisha.
D Kuona neema mbalimbali tulizopewa.
E Kuonesha madhara ya kumuasi Mungu.



Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

CamScanner

(xiv) Kwa nini Mtume (S.A.W) aliwaamrisha Maswahaba wake kuhama kutoka Makka kwenda Madina mwaka wa 13 B.U?

A Kufunguka kwa hali ya kibiashara katika mji wa Madina wakati huo.
B Hitaji la Waislamu kupata sehemu nzuri ya kuishi kwa amani na utulivu.
C Hitaji la Waislamu kuishi katika sehemu yenye huduma nzuri za kijamii.
D Hitimisho la mikataba ya Aqaba baina ya Waislamu na watu wa Madina.
E Kuongezeka kwa ushindani wa kibiashara katika mji wa Makka.

(xv) Mtiririko upi unabainisha kwa usahihi ujumbe wa Mwenyezi Mungu (S.W) kwa Mtume wake (S.A.W) uliokusudia kumuandaa kimafunzo?

A Suratul Alaq, Suratul Fat'ha na Suratu Muddathir
B Suratul Alaq, Suratul Muddathir na Suratu Muzammil
C Suratul Alaq, Suratul Muzammil na Suratu Muddathir
D Suratul Alaq, Suratul Muzammil na Suratul Fat'ha
E Suratul Muzzammil, Suratul Alaq na Surat Mudatthir

2. Oanisha Funga za Sunna zilizopo katika **Orodha A** na majina ya Funga hizo katika **Orodha B** kisha andika herufi ya jibu sahihi kwa kila kipengele katika kijitabu chako cha kujibia.

| Orodha A | Orodha B |
|---|---|
| (i) Kufunga terehe 12, 13 na 14 katika miezi ya Hijriya. | A. Funga ya Ashura |
| (ii) Kufunga tarehe 9 katika mwezi wa Dhul Hijja. | B. Funga ya kafara |
| (iii) Kufunga tarehe 10 katika mwezi wa Muharram. | C. Funga Siku nyeupe |
| (iv) Funga *muakkada* kila mwezi wa 10 Hijriya. | D. Sunna Nabii Dawud |
| (v) Kufunga kila baada ya siku moja. | E. Sitta Shawwal |
| | F. Funga ya Arafa |
| | G. Masiku meusi |

**SEHEMU B (Alama 35)**

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

3. Kwa kutumia hoja tano, bainisha udhaifu wa madai kuwa Mtume (S.A.W) alifundishwa Qur'an na watu.

4. Ndugu Masudi alionekana akifanya maovu hadharani kwa mujibu wa Uislamu na alipokumbushwa alidai kuwa anafanya hivyo kwa kuwa ni Qadar. Kwa kutumia hoja mbili, muelimishe kwa kukanusha madai yake.

5. Pendekeza njia tano zitakazowezesha taasisi ya ndoa katika jamii ya sasa kufikia malengo yake kimalezi na kuimarisha maadili mema kwa watoto.

6. Fafanua sababu mbili za kuporomoka kwa Dola ya Kiislamu aliyoiacha Mtume (S.A.W).



Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org
CamScanner

7. Ili Shahada ya mtu ikamilike ni lazima kumshuhudia Mtume (S.A.W) katika Shahada ya pili. Bainisha sababu mbili za kufanya hivyo.

8. Tofautisha mfumo wa uchumi wa Kiislamu na mifumo waliyobuni watu katika dhana zifuatazo:
   (a) Dhana ya umiliki wa mali
   (b) Dhana ya matumizi ya mali

9. Watu waovu katika zama hizi wanatumia kivuli cha Dini ya Kiislamu kueneza vurugu na vita katika jamii mbalimbali wakificha malengo yao ya kiuchumi na kisiasa. Bainisha sifa mbili zinazoonesha ubatili wa vita au vurugu hizo kwa mujibu wa mafundisho sahihi ya Uislamu.

## SEHEMU C (Alama 45)

Jibu maswali **matatu (3)** kutoka sehemu hii.

10. Eleza sababu tano za Waislamu kulazimika kusimamisha Sala tano kila siku katika maisha yao yote hapa duniani.

11. Maswahaba (R.A) walipokea Sunnah ya Mtume (S.A.W) kwa umuhimu mkubwa katika maisha yao ingawa hawakuandika kwa wingi. Eleza sababu nne zilizosababisha kuwa na uandishi duni wa Hadithi wakati wa Mtume (S.A.W).

12. Qur'an imeteremshwa kwa kiarabu ili kuwa mwongozo kwa viumbe wote. Kwa kutumia hoja tatu, eleza namna ambavyo ujumbe wake utawafikia wasiokuwa waarabu na wasiojua lugha hiyo.

13. Mkataba wa Madina ulilenga kuimarisha mahusiano na mshikamano baina ya Waislamu na kuweka misingi ya mahusiano mema kati yao na watu wa imani nyingine. Thibitisha hoja hii kwa kuonesha namna mkataba huo ulivyoimarisha mahusiano baina ya pande zote mbili (Toa hoja mbili kila upande).



Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

CamScanner